



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO



Simu Na. +255(028) 2820137  
Fax Na. +255(028) 2820137  
E-mail: ded@kakonkodc.go.tz  
Tovuti: www.kakonkodc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
S.L.P 03,  
KAKONKO.

**Unapojibu tafadhali taja:**  
Kumb.Na. HW/KNK/S. 40/VOL. II/30

21.04.2023

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko anayo furaha kutangaza nafasi 3 za ajira ya kudumu kwa watanzania wote wenye sifa stahiki kwa nafasi ya **dereva daraja la II nafasi 3**. Nafasi za ajira hizi zinatokana na kibali kibali cha Ajira kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora** kwa barua yenye Kumb. Na. FA.97/228/01"TEMP"/06 cha tarehe 06 Aprili, 2023. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04/05/2023 saa tisa na nusu alasiri. Maombi yote yatamwe kwa njia ya posta kwa kutumia anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P. 03,  
KAKONKO.

**1. Dereva daraja la II – Nafasi 03**

**Kazi na Majukumu**

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- Kufanya usafi wa gari.
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

## Sifa za Kuajiriwa.

- Mwombaji awe na Cheti cha Kidato cha Nne Form IV au VI.
- Mwombaji awe na leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Mwombaji awe amehudhuria mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Mwombaji atakayekuwa na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza

## MASHARTI YA JUMLA

Mwombaji anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo kikamilifu.

- (i) Awe ni Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45, bila kujali jinsi ulemavu, kabila, dini au hali.
- (ii) Aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na Maelezo Binafsi (CV) yaliyojitosheleza kwa maana ya taarifa na mawasiliano. Pia aambatanishe picha 1 "Passportsize" iliyochukuliwa hivi karibuni na nakala za vyeti vya Taaluma (Academic) na Weledi (Professional). Transcript "Testimonials" na " Provisional Results" au Statement of Results havipokelewi.
- (iii) Maombi yawasilishwe kabla au mnamo tarehe 04/05/2023 saa 9:30 Alasiri. Maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe na muda uliopangwa hayatafanyiwa kazi.



Ndaki S. Mhuli  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
KAKONKO.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KAKONKO

## NAKALA:-

Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
S.L.P 2320,  
DODOMA.

**NB: Tangazo hili linapatikana pia kupitia tovuti ya HALMASHAURI:**  
**[www.kakonkodc.go.tz](http://www.kakonkodc.go.tz)**